

Swahili A: literature – Higher level – Paper 1
Swahili A : littérature – Niveau supérieur – Épreuve 1
Swahili A: literatura – Nivel superior – Prueba 1

Wednesday 10 May 2017 (afternoon)
Mercredi 10 mai 2017 (après-midi)
Miércoles 10 de mayo de 2017 (tarde)

2 hours / 2 heures / 2 horas

Instructions to candidates

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a literary commentary on one passage only.
- The maximum mark for this examination paper is **[20 marks]**.

Instructions destinées aux candidats

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Rédigez un commentaire littéraire sur un seul des passages.
- Le nombre maximum de points pour cette épreuve d'examen est de **[20 points]**.

Instrucciones para los alumnos

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un comentario literario sobre un solo pasaje.
- La puntuación máxima para esta prueba de examen es **[20 puntos]**.

Andika uchambuzi kuhusu kifungu **kimoja** kati ya hivi:

1.

Kero la uchungu lililokuwa kifuani mwake lilimchachafya, likamfanya kupukutika machozi kupu kupu pale alipokaa. Aliwaza jinsi alivyotaribu kumshawishi babake ili aweze kuelewa dhamira yake lakini akawa haambiliki hasemezeki. Kushindana naye hakungefaa chochote, kwa hivyo akaamua kuchukua hatua aliyochukua ya kutoroka. Naam, lisilo budi hutendwa. Hangekimbililia
5 kwa shangaziye Bi. Namvua kwani huyu, kama alivyo babake, alishikilia yale yale yaliyomtimua kwao. Mjomba wake, Bwana Yusufu tu ndiye ambaye angemwelewa lakini huyu aliishi mtaa wa Mkwajuni, mwendo wa maili kumi kutoka kwao. Hangeweza kwenda huko peke yake. Isitoshe, mtaa huo ulikuwa na wakora wengi mno ambao aghalabu waliwavizia wapita njia na kuwaporu mali yao. [...]

10 Kwa hivyo, kimbilio lake lilikuwa kwa Shabani ambapo aliamini kwamba jamaa hii ingemwelewa na kumsaidia. Alitaka pia kukaa na bintiamu yake, Riziki, ambaye alikuwa likizoni baada ya shule kufungwa kwa likizo ndefu ya krismasi. Riziki alijitambulisha kuwa msichana mzuri sana kwa tabia na bidii masomoni. Tumaini alitaka kumwiga bintiamuye kwa kila hali ili naye pia aweze kujiunga na shule ya upili baada ya kukamilisha masomo ya
15 elimu ya msingi. Aliwaza jinsi Riziki alivyomsimulia maisha katika shule ya bweni alikosomea. Alimwomba Mungu amfungulie njia abanduke katika shida zilizomzonga.

Mara alisikia kukuru kakara kutoka mbali. Kelele hizo kama za gari, zilikuwa zikimjia kwa kasi sana. Hakuweza kujizuia pale alipokaa. Kwa mshtuko mkubwa huku moyo ukirindima kifuani mwake, aliruka kama mkizi. Alitumbua macho utadhani alimwona ibilisi mwenyewe
20 kutokana na hofu kuu iliyomvaa. Huku kifurushi kikiwa mikononi, alijirusha kwenye gugu lililokuwa nyuma ya ule mpapai. Alizidi kutumbua macho, huku moyo ukimwenda mbio. Hapo alimwona mzegazega akipita mbio huku amebeba madebe shinda. Nyuma yake, alifuatiwa na kijana mnene mwenye misuli, aliyesukuma rukwama lililosheheni madebe shinda vilevile. Wote walikuwa mbioni utadhani maji yatakauka kisimani walikokuwa wakielekea.

25 Kwa kawaida vijana hao huyajaza madebe maji kisha wakayatembeza mitaani huku wakinadi "Haya maji, haya maji!" kwa wale waliokuwa wazembe wa kuteka maji kisimani. Tumaini alijizoa kutoka pale alipojificha na kulikaribia jiwe lake tena akajiketia. Kilimpitikia kicheko kwani alijiona mwoga sana kutokana na jinsi alivyokuwa akitetemeka, huku mate yamemkauka mdomoni. Hata hivyo, alijua kuwa punde jua lingepasua mbingu kwani hata jogoo
30 alikuwa anawika sasa. Tumaini alijisemea kimoyomoyo, "uso unacheka, lakini moyo unalia".

Alipokuwa akifikiri jinsi atakavyomkabili mamake mdogo, mara alishtukia lile jiwe alilokalia likisogea taratibu! Kwa ghafla aliruka huku akilikodolea macho jiwe ambalo lilionekana jeusi lakini likiwa mwendoni. "Ama kweli, haya ni maajabu ya Musa," alijisemea kimoyomoyo. Kumbema! Hakuwa ameketia jiwe bali mzee kobe ambaye sasa alitaka kuanza siku yake
35 kujitafutia riziki. "Pengine kobe huyu alichoka kuketiwa, akaamua liwe liwalo, angejitahidi kujiauni," aliwaza Tumaini. Kobe alitoa kichwa chake nje na kuirefusha shingo yake. Taratibu, alitambaa kwenye nyasi na kupotelea kwenye gugu nyuma ya ule mpapai.

Tumaini alizidi kupatazama mahali alipojipenyeza kobe huku akiwaza kuwa hali yake ilikuwa mbaya zaidi kushinda ya kobe huyo kwani hakujua yale yaliyokuwa mbele yake au
40 hata maisha yake ya baadaye. Kwa upande wake, kobe alikuwa tayari yumo katika harakati za kujitafutia riziki kokote kule, na usiku ukiwadia, angejipenyeza mahali na kuupumzisha mwili wake. Hakuwa na wasiwasi wowote kama wake kwamba angekula nini, angesoma lini au angetafuta kazi wapi. Kwa muda kidogo, Tumaini alitamani kuwa kobe au hata ndege wa angani arukaye na kujitafutia riziki yake bila wasiwasi.

- 45 Alipokuwa akiwazia hilo, alitupa jicho upande wa nyumba ya Shabani na kumwona mamake mdogo akifululiza kuelekea kwenye banda la ng'ombe, birika mkononi. Tumaini alifahamu kuwa bibi huyo alikusudia kumkama ng'ombe wake ili apate maziwa ya kutayarishia staftahi. Je, amfuate pale bandani au amsubiri amalize shughuli ile kwanza? Potelea mbali. Tumaini ambaye sasa alihisi baridi ile ya alfajiri kutokana na gauni jepesi alilovaa, aliamua
- 50 kumwendea Bi. Halima mle bandani. "Yatakayofuata yana Mungu," alijisemea kimoyomoyo. Alivuta hatua kuelekea bandani. Alijihisi mchovu na usingizi sasa ulikuwa umesharabu machoni mwake. Hata hivyo, haikumwia vigumu kuuona uchengu wa majilio ya alfajiri na hamu kubwa ya kuyasimulia yale yaliyoutia moyo wake simanzi.

Clara Momanyi, *Tumaini* (2006)

2.

Cha Kuvunja Hakina Rubani

Chombo cha kuvunda, hakina rubani,
Ukaona chenda, ukatumaini,
Mara kitapanda, kishie mwambani,
Hakina rubani, chombo cha kuvunja.

5 Nawe maarufu, mahika sukani,
Nahodha mongofu, msoma ramani,
Huja hitilafu, iwe kisirani,
Hakina rubani, chombo cha kuvunja.

10 Japo ni oshari¹, chatoka mangoni,
Kisicho athari, wala nukusani,
Hufiki bandari, wala kivukoni,
Hakina rubani, chombo cha kuvunja.

15 Shuari na iwe, kisafiri ndani,
Na kusiwe kuwe, Lamu² na kipini,
Ni kama sunguwe³, hushia taoni,
Hakina rubani, chombo cha kuvunja.

20 Hata cha msaji⁴, mbao nambawani,
Kisovuja maji, muundo wa fani,
Chombo kivunjaji, huvunja nangani,
Hakina rubani, chombo cha kuvunja.

Aliloandika, Mola Rahamani,
Likitaka fika, la baa jamani,
Huwezi lepuka, hata fanya nini,
Hakina rubani, chombo cha kuvunja.

25 Tamati nafunga, tosha wastani,
Huwezi kupinga, la Mola Manani,
Wala huna kinga, kuwa salamani,
Hakina rubani, chombo cha kuvunja.

Said Karama, *Utunzi Wenye Fahari* (1986)

¹ oshari: mpya

² Lamu: mji katika pwani ya Kenya

³ sunguwe: jina la mahali baharini

⁴ msaji: aina ya mti